# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZILIZOPATA KIBALI CHA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA NA UTAZAMAJI WAKATI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE WA JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA

Dodoma, 17 Agosti, 2023

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 17 Agosti, 2023, imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mdogo wa Ubunge wa Jimbo la Mbarali na Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara kwa asasi za kiraia tatu (3). Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, inayoipa Tume jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo. Orodha ya asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na maeneo watakayotoa elimu hiyo, imeoneshwa katika jedwali lifuatalo: -

| NA. | JINA LA ASASI YA KIRAIA | HALMASHAURI | JIMBO/KATA |
|---|---|---|---|
| 1. | Umbrella of Women and Disabled Organisation (UWODO) | Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | Mtyangimbole |
| 2. | Alpha and Omega Reconciliation and Peace Building (AREPEB) | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali | Mbarali |
| 3. | Bright Child Development Tanzania (BRIGHT CHILD) | Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi | Mwaniko |

Aidha, katika utekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura, asasi hizo zitapaswa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020 katika kipindi chote cha kutoa elimu hiyo katika uchaguzi mdogo.

Vilevile, Tume imetoa kibali cha utazamaji wa uchaguzi kwa asasi ya kiraia ya Bridge Development Trust Organization (BRIDETO) ambayo iliomba kutazama uchaguzi mdogo wa Madiwani katika Kata ya Mwaniko iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na Kata ya Nala katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia kanuni ya 16(5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020.

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi mdogo iliyotolewa na Tume, uteuzi wa wagombea katika uchaguzi huo utafanyika tarehe 19 Agosti, 2023. Aidha, kuanzia tarehe 20 Agosti hadi tarehe 18 Septemba, 2023 kitakuwa ni kipindi cha kampeni kwa vyama vya siasa na wagombea. Uchaguzi utafanyika siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023.

Tume inatumia fursa hii kuzipongeza asasi zote za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na utazamaji wa uchaguzi. Vile vile inazikumbusha asasi hizo kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, kibali hiki kitatumika kuanzia tarehe 18 Agosti, 2023 hadi tarehe 18 Septemba, 2023.

Imetolewa na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**